

Maswali

1. Sauli alimtii Mungu?
2. Mungu alimwambia Samweli amuendee nani?
3. Samweli alikutanaje na Yese?
4. Samweli alifikiria nini juu ya Eliabu?
5. Mungu alisema nini?
6. Mwanzoni Samweli aliona wana wa Yese wangapi?
7. Mwana mdogo wa Yese alikuwa wapi?
8. Mungu alisema nini juu ya Daudi?
9. Sauli alijisikiaje?
10. Daudi alifanya kazi gani?

Majibu

1. Sauli hakumtii Mungu.
2. Mungu alimwambia Samweli aenda kuona Yese.
3. Samweli alikutana na Yese alipomkaribisha kwa kutoa dhabihu.
4. Samweli alifikiria Eliabu ndiye anafaa.
5. Mungu alisema, “sijali vile watu wanaonekana - ninaangalia mioyo yao”.
6. Mwanzoni Samweli aliona wana wa Yese 7.
7. Mwana wa Yese mdogo alikuwa anachunga kondoo.
8. Mungu alisema, “Mpake mafuta, nimemchagua yeye”.
9. Sauli alikuwa na huzuni, alitaka kusikiliza muziki.
10. Daudi alifanya kazi tatu; alicheza kinubi, alibebea Saulu silaha na kuchunga kondoo wa Yese.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



13 Daudi anatiwa mafuta

Marejeo

1 Samweli 16

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu alimchagua Daudi kuwa mfalme, tena Mungu humchagua mtu kwa ajili ya moyo wake.

Maneno maalum

1. Sauli hakutii + Mungu akamkataa
2. Mwana wa Yese atakuwa mfalme.
3. Eliabu + Mungu huangalia moyo
4. Wana 7 + hakuchagua yeyote + mwana mdogo anachunga kondoo.
5. Tiwa mafuta + Daudi + Mungu alikuwa naye.
6. Daudi hakufurahi + alitaka muziki
7. Daudi alicheza kinubi + mchukua silaha + mchungaji

13.1 Sauli hakumtii Mungu kwa hivyo Mungu alimkataa. Mungu alimwambia Samweli asione vibaya kwa sababu alikuwa amechagua mtu mwingine kuwa mfalme.

13.2 Mungu alimwambia Samweli aende amuone Yese. Alimwambia, "Nimechagua mwana wake mmoja awe mfalme." Samweli aliogopa kwamba Sauli atatambua alichokuwa akifanya. Kwa hivyo Mungu alimwambia afanye dhabihu ya n'gombe na amkaribishe Yese.


13.3 Eliabu mwana wa Yese wa kwanza aliletwa mbele ya Samweli. Samweli alimwalia na akaona anafaa kuwa mfalme mzuri. Lakini Mungu alisema, "Mimi siangalii kibinadamu. Mimi naangalia moyo wa mtu."

13.4 Yese alileta wana wake 7 mbele ya Samweli.

Hakuna aliyechakuliwa na Mungu.

Halafu Samweli akauliza, "Una mwana mwingine aliyebaki?"

Yese akasema, "Mwana wangu mdogo ako anachunga kondoo." Samweli akasema, "Enda umulete."



13.5 Wakati kijana mdogo alifika, Samweli aliona kwamba anafaa. Mungu alisema, "Mpake mafuta, ndiye huyu!" kijana alitwa Daudi. Tangu siku hiyo Mungu alikuwa naye.

13.6 Wakati huo Sauli, hakukuwa na furaha. Alitaka mtu wakumtuliza. Akataka mtu wa kumchezea muziki. Daudi alichaguliwa kwa sababu alijua kucheza kinubi.



13.7 Sauli alimpenda Daudi sana. Alipomchezea kinubi Sauli alijihisi vizuri. Alimtaka Daudi akae naye kwa hivyo alimfanya mchukuwa silaha pia. Wakati mwingine alimuacha Sauli na kwenda kuchunga kondoo wa baba yake.